TANGAZO LA SERIKALI NA. 529 la Tarehe 10/07/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) (g) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA ( ADA ZA VIBALI VYA BURUDANI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI ZA MWAKA, 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi za Mwaka,2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi;

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo;

*"ada"* maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii.

"Halmashauri"maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Moshi;

"kibali cha burudani" maana yake ni kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa ajili ya

kufanya shughuli za burudani ambayo inakutanisha watu katika ukumbi, uwanja wa michezo au sehemu yoyote ya wazi au mitaani;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni malipo ya fedha taslimu zinazolipwa na mtu anayehitaji huduma. "wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi.

Kibali

4. (1) Kila mtu au taasisi yeyote isiyokuwa ya kiserikali au kidini itakayoendesha shughuli za burudani, italazimika kuomba kibali na kulipia kibali cha kuendesha shughuli hiyo kutoka Halmashauri kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kibali hicho kitaonesha-

(a) sehemu itakayofanyika shughuli hiyo;

(b) muda wa kuanza na kumalizika kwa shughuli hiyo;

(c) aina ya Shughuli au burudani.

(3) Nakala ya kibali hicho itapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ikiwa na viambatisho vyote husika.

Marufuku

5. (1) Ni marufuku kwa mwenye ukumbi wa video, sinema au sehemu yoyote kuonyesha picha za video ambazo hazina maadili.

(2) Ni marufuku kwa watoto wadogo, wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) kuingia katika kumbi za burudani au muziki.

Wajibu

6. (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa ukumbi wa mziki kupiga muziki kwa kiwango cha sauti cha kawaida bila kuathiri watu wanaozunguka eneo la ukumbi huo wa muziki.

(2) Kila mwonesha video au sinema atatakiwa kuweka sauti ya chini wakati wa onesho bila kuathiri majirani wanaomzunguka.

(3) Ni wajibu wa kila mmiliki wa kumbi za burudani au bar au mziki kuhakikisha wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) haingii katika kumbi izo na endapo itabainika kuingia kwa wanafunzi au watoto hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mmiliki wa kumbi hizo.

Uwezo wa afisa mwidhiniwa

7. Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika ukumbi wowote wa burudani, sinema au sherehe yeyote inayofanyika mtaani na hadharani kukagua kibali kinachoruhusu uendeshaji wa shughuli hiyo.

Kibali maalum

8. Mtu au kikundi chochote kitakachofanya sherehe katika mitaa au viwanja vya wazi itabidi apate kibali cha kufunga barabara ya mtaa.

Muda wa burudani

9. (1) Muda wa kuonesha video au sinema utakua

ni siku ya jumamosi na jumapili kuanzia saa saba mchana hadi saa kumi na mbili jioni.

(2) Disko litaruhusiwa kupigwa siku ya ijumaa hadi jumapili kuanzia saa tatu usiku hadi saa tisa usiku.

Kufililisha kosa

10. Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari yake mwenyewe kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini na kodi anayodaiwa chini ya Sheria Ndogo hii na kulipa kiasi kisichopungua shilingi laki mbili(Tsh. 200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (Tsh. 500,000/=).

Makosa

11. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote endapo-

(a) atapiga mziki unaosababisha kero kwa majirani;

(b) atafanya sherehe yoyote bila kupata kibali.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilling laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shillingi millioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 4 (1))*

SEHEMU "A"

Ada ya kusajili kikundi cha sanaa na muziki Tsh 30,000/= kwa mwaka

SEHEMU "B"

KIBALI CHA DISKO KWA SIKU MOJA

i. kikundi cha ndani ya Halmashauri ya Wilaya Tsh 30,000/=
ii. kikundi cha nje ya Halmashauri ya Wilaya lakini ndani ya Mkoa Tsh 50,000/=
iii. kikundi cha nje ya Mkoa Tsh 80,000/=

SEHEMU 'C"

KIBALI CHA KUPIGA DANSI SIKU MOJA

i. kikundi cha ndani ya Halmashauri ya Wilaya Tsh 30,000/=
ii. kikundi cha nje ya Halmashauri ya Wilaya lakini ndani ya Mkoa Tsh 50,000/=
iii. kikundi cha nje ya Mkoa Tsh 80,000/=

SEHEMU "D"

KIBALI CHA KUONESHA SANAA ZA MAONYESHO

(semina, video, maigizo,sarakasi, ngumi, ngoma , kunyanyua vyuma, n.k)

i. ada ya video au sinema kwa mwaka
   (a) ukumbi usiozidi watu 350 ada ni Tshs 300,000/=
   (b) ukumbi unaochukua watu 351-550 ada ni Tshs 500,000/=
   (c) ukumbi unaochukua watu 551-750 ada ni Tshs 700,000/=
   (d) ukumbi unaochukua watu 751 na kuendelea ada ni Tshs 1,000,000/=
ii. kikundi cha ndani ya wilaya Tshs 50,000/= kwa siku
iii. kikundi toka nje ya Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya lakini ndani ya Mkoa Tsh 60,000/= kwa siku.

SEHEMU "E"

kibali cha kuuza dawa za asili Tsh 50,000/= kwa mwaka

SEHEMU "F"

KIBALI CHA KUENDESHA TIBA ZA ASILI NDANI YA ENEO LA HALMASHAURI YA WILAYA

i. Toka nje ya Halmashauri ya wilaya Tsh 50,000/= kwa mwaka
ii. Waganga maarufu ndani ya Halmashauri ya Wilaya Tsh 100,000/= kwa mwaka
iii. Waganga wadogo ndani ya Halmashauri ya Wilaya Tsh 50,000/=

SEHEMU "G"

ADA KWA AJILI YA KUZURU SEHEMU ZA KIHISTORIA KWA MTU MMOJA

| Muhusika | Raia TSh | Asiye raia USD |
|---|---|---|
| Mtu mzima | 2,000/= | USD 5 |
| Wanafunzi wa shule za msingi | Bure | USD 2 |
| Taasisi | 25,000/= | USD 10 |

SEHEMU "H"

Ada kwaajili ya kumbi za starehe katika maeneo ya mjini kwaajili ya shughuli za maonyesho,starehe,(social clubs and halls), viwanja vya michezo,(stadium)ambavyo hutumika kwa kutoza viingilio kila mwaka itazingatia SEHEMU "D" kipengere cha (i)

SEHEMU "I"

KIBALI CHA KUNASA NYIMBO ZA ASILI, UPIGAJI PICHA VITU NA VIKUNDI VINAVYO JISHUGHULISHA NA FANI ZA KITAMADUNI KWA MARA MOJA

| Raia TSh | Asiye raia USD |
|---|---|
| 300,000/= | USD 200 |

SEHEMU "J"

Kibali cha kuendesha mashine za michezo ya kubahatisha kwa mwaka Tsh 120,000/= kwa mashine moja iliyosajiliwa na Bodi ya Michezo ya Bahati Nasibu ya Taifa na kupewa kibali.

SEHEMU "K"

Kibali cha kuchezesha michezo ya mipira ya miguu kwa kutoza viingilio kwenye viwanja vya michezo (stadium) kokote kule ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya itakuwa Tsh 50,000/= kwa timu za ndani ya Halmashauri ya Wilaya na Tsh 100,000/= kwa timu zitakazo toka nje ya Halmashauri ya Wilaya na Mkoa.

SEHEMU "L"

Kibali cha kuendesha shughuli zozote za mikutano ya kidini nje ya maeneo ya makanisa au misikiti bure (lakini lazima kibali kitolewe)

SEHEMU "M"

Kibali cha kuendesha shughuli zozote za kiutamaduni ambazo hazikutajwa hapo juu ni Tsh 25,000/=

SEHEMU "N"

Kibali cha kuendesha michezo ya mashindano ya magari, pikipiki ndani ya Halmashauri ya Wilaya itakuwa ,kila gari litalipiwa shilingi 20,000/= na kila pikipiki italipiwa shilingi 15,000/= kwa siku.

JEDWALI LA PILI

HATI YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 10)*

Mimi ……………………………………………………………..……..nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………………….ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kwamba mnamo tarehe ………………ya Mwezi …………….Mwaka……………………………………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………………cha Sheria Ndogo ya (Ada za Burudani) za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi za Mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha ada/ ushuru ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………..ya Mwezi………………..Mwaka …………………

*Jina*…………………………………………………….....

*Saini*…………………………………………….………….

Mbele ya :

Jina: ……………………………………………

Cheo: …………………………………………

Saini: ……………………………………………

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi umebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kwa Azimio la kikao cha Halmashauri kilichoitishwa na kufanyika tarehe 29/2/2019, na ilifanyika mbele ya:-

KASTORI G. MSIGALA,
*Mkurugenzi Mtendaji*,
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Moshi*

MHE. MICHAEL S. KILAWILA,
*Mwenyika,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Moshi*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
27 Desemba, 2019

MHE. SELEMANI S JAFO (MB.),
*Waziri-OR-Tamisemi*